VIFUPISHO

AIDS	-	Acquired Immunodefficiency Syndrome
ASDP	-	Agriculture Sector Development Program
BMU	-	Beach Management Unit
BRN	-	Big Results Now
CD	-	Compact Disc
CDCF	-	Council Development Catalyst Fund
CDG	-	Capital Development Grant
CDR	-	Cummulative Development Report
CG	-	Central Government
CHMT	-	Council Health Management Team
DCC	-	District Consultative Committee
DVD	-	Digital Video Disc
EASTC	-	East Africa Statistical Training College
EPICOR	-	Mfumo wa Uandaaji wa Taarifa za Fedha
HIV	-	Human Immunodefficiency Virus
ICT	-	Information and Communication Technology
IDSR	-	Integrated Disease Surveillance and Response
IFMS	-	Intergrated Financial Management System
IPSAS	-	Intrenational Public Sector Accounting Standard
KM	-	Kilometer
LGMD	-	Local Government Monitary Database
KCMC	-	Kilimanjaro Christian Medical Centre
LAAC	-	Local Authorities Accounting Committee
MDA	-	Mass Drug Administration
MEMKWA	-	Mpango wa Elimu ua Msingi kwa walioikosa
MKUKUTA	-	Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania
MMAM	-	Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi
MSD	-	Medical Store Department
MoFP	-	Ministry of Finance and Planning
MTUHA	-	Mfumo wa Taarifa ya Uendeshaji wa Huduma za Afya
MUKEJA	-	Mpango wa Uwiano Kati ya Elimu ya Watu Wazima na Jamii
NHIF	-	National Health Insurance Fund
NMSF	-	National Multisectoral Strategic Framework
O & OD	-	Opportunities and Obstacles to Development
OC	-	Other Charges

OPD	-	Out Patient Development
OS	-	Own Source
PE	-	Personal Emoluments
P4P	-	Pay For Performance
P0-RALG	-	President's Office Regional Administration and Local Government
SACCOS	-	Savings & Credits Cooperative Society
REC	-	Reach Every Child
RCC	-	Regional Consultative Committee
R & R	-	Mfumo wa Kutoa Taarifa za Afya
SEDP	-	Secondary Education Development Program
TACAIDS	-	Tanzania Commission For AIDS
TAMISEMI	-	Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa
TASAF	-	Tanzania Social Action Fund
TIB	-	Tanzania Investment Bank
TIKKA	-	Tiba kwa Kadi
TOMSHA	-	Tanzania Output Monitoring System For Non - Medical HIV and AIDS Interventions
TRC	-	Teacher's Resource Center
TSCP	-	Tanzania Strategic Cities Project
TSS	-	Takwimu za Shule za Sekondari
TT	-	Chanjo ya Pepopunda
UMITASHUMTA	-	Umoja wa Michezo na Taaluma Shule za Msingi Tanzania
UMISSETA	-	Umoja wa Michezo na Sanaa Shule za Sekondari Tanzania
WDC	-	Ward Development Committee
WDF	-	Women Development Fund
WAVIU	-	Watu Wanaoishi na Virusi Vya UKIMWI
WEO	-	Ward Executive Officer
YDF	-	Youth Development Fund
O&M	-	Operation and Maintanance

HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA

MUHTASARI WA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2022/2023

1.0: UTANGULIZI:

Mhe. Mwenyekiti, Wajumbe wa Baraza la Madiwani.

Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuwa hai hadi siku hii ya leo. Naomba kuwasilisha rasimu ya Mpango na Bajeti ya Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2022/2023. Mapendekezo haya yameandaliwa kwa kuzingatia Mwongozo wa Bajeti unaotamkwa kwenye Sheria ya Bajeti Namba 11 ya Mwaka 2015 pamoja na kuzingatia masuala yafuatayo:-

i. Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa Mwaka 2021/2022 – 2025/2026;
ii. Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025;
iii. Hotuba ya Mhe. Rais wa Awamu ya Sita wakati wa akilihutubia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
iv. Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) 2020-2025;
v. Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 -2025;
vi. Mwongozo wa Bajeti uliotolewa na Wizara ya Fedha na Mipango wa Mwaka wa Fedha 2022/2023;
vii. Maelekezo ya Kamati za Kudumu za Halmashauri;
viii. Maelekezo na ushauri kutoka Sekretarieti ya Mkoa wa Mwanza;
ix. Sera Mbalimbali za kisekta;
x. Maoni ya Wadau mbalimbali wa maendeleo katika Halmashauri;

Mhe. Mwenyekiti, Kabla ya kuwasilisha Mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi na Mpango na Bajeti ya Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, naomba kuwasilisha dondoo muhimu kuhusu Mpango na Bajeti ya Mwaka 2022/2023;

A. Mapato

Makisio ya Mapato yanayotokana na vyanzo vya ndani yameongezeka kutoka Tsh. 10,172,706,000.00 kwa Mwaka wa fedha 2021/2022 hadi Tshs 13,524,000,000.00 kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 sawa na ongezeko la asilimia 32.9. Hii inatokana na:-

i. Halmashauri kuanza kutumia na kutekeleza sheria ndogo mpya zilizoboreshwa zinazoipa uwezo wa kukusanya mapato kwa nguvu ya kisheria sambamba na kuchukua hatua zaidi za kisheria kwa wanaoshindwa kulipa ada na tozo mbalimbali za Halmashauri;
ii. Kuendelea kuimarika kwa takwimu mbalimbali za vyanzo vya mapato zoezi linaloendelea kwa sasa ikiwa ni pamoja na kuwatambua wafanyabiashara wote wadogo kwa wakubwa ili waweze kulipa kodi ya huduma kama ilivyobainishwa katika sheria ndogo.
iii. Uwepo wa ongezeko la ukusanyaji kwa baadhi ya vyanzo vya mapato kutokana na matumizi ya mfumo wa kielektroniki katika usimamizi na ufuatiliaji wa mapato;
iv. Kutoa elimu ya kodi kwa wananchi ili kuinua ari ya ulipaji kodi (ushuru);
v. Usimamizi na utekelezaji wa mikataba ya ukusanyaji mapato; na
vi. Kuundwa kwa timu maalumu za ufuatilialiaji Mapato ikiwa ni pamoja na kuajiri vibarua kwa ajili ya kuongeza nguvu ya ukusanyaji mapato.

B. Mishahara

Bajeti ya Mishahara imeongezeka kutoka **TShs 42,496,789,508.00** kwa Mwaka **2021/2022** hadi **TSh. 42,819,341,512.00** kwa Mwaka **2022/2023** sawa na ongezeko la **0.8%.** Ongezeko hili linatokana na ajira mpya, upandishwaji wa madaraja na vyeo kwa Watumishi wa kada mbalimbali.

C. Matumizi ya Kawaida(Other Charges)

Makisio ya Matumizi ya Kawaida yamezingatia Ukomo wa Bajeti wa Mwaka wa Fedha 2021/2022. Hata hivyo mabadiliko yanaweza kutokea endapo ukomo huo utabadilika kwa kuzingatia maelekezo yatakayotolewa na Serikali Kuu. Kwa sasa maelekezo ya kutumia Makisio ya **Tshs 1,727,568,000.00** kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 yamezingatiwa katika Mpango na Bajeti hii.

D. Miradi ya Maendeleo

Ukomo wa Bajeti ya Mifuko mbalimbali mathalani Mfuko wa Pamoja wa Afya (HSBF), Global Fund, EP4R, TASAF na Mfuko wa Jimbo (CDCF) pamoja na fedha zingine kutoka Serikali Kuu (Ujenzi wa Hopitali, ujenzi wa jengo la Utawala) na Miradi ya Kimkakati ni sawa na za Mwaka huu wa Fedha 2021/2022 unaoendelea.

- ✓ Fedha zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo kutoka mapato ya ndani ni 60% ya mapato yote ya ndani ni Tshs 7,506,367,440.00 ukilinganisha na mwaka wa fedha 2021/2022 ambapo ilikuwa ni Tsh5,576,516,400.00

- ✓ Bajeti ya miradi imeelekezwa kukamilisha miradi viporo, na miradi yote ya ujenzi inayolenga jamii moja kwa moja hususani sekta za Elimu, Afya Barabara, sekta ya Uvuvi pamoja na Masoko kwa lengo la kuongeza wigo wa ukusanyaji wa mapato.

E*. Maandiko ya Miradi*

Sambamba na uwasilishaji wa Mapendekezo ya Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Halmashauri pia imewasilisha Andiko la Mradi wa Viwanda Nyamhongolo kwa ajili ya ujenzi wa Miundombinu ya barabara. Pia maandiko mengine ni Ujenzi wa Kituo cha Kibiashara Buzuruga (Buzuruga Commercial Centre) baada ya standi kuhamishiwa eneo la Standi Kuu ya Mabasi Nyamhongolo na Ujenzi wa Chuo cha Afya Kabusungu katika eneo la Hospitali ya Wilaya.

2.0 Mapitio ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2020/2021

2.1 Mapato na Matumizi ya Halmashauri kwa Mwaka 2020/2021

2.1.1 Mapato

Katika kipindi cha Mwaka **2020/2021** Halmashauri ilipanga kukusanya/kupokea jumla ya **Tshs. 62,802,273,008.00** kwa kutekeleza shughuli mbalimbali za Maendeleo na Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021, jumla ya

Tshs 58,342,566,438.00 zilipokelewa/zilikusanywa kutoka vyanzo mbalimbali hii ni sawa na asilimia **93** ya lengo kwa mchanganuo ufuatao:-

Machanganuo wa Mapato ya fedha kwa mwaka 2020/2021

Na	Chanzo	Makisio 2020/2021	Mapato halisi 2020/2021	%
1.	Mishahara(PE)	35,418,015,337.00	34,277,465,500.00	97
2.	Matumizi ya Kawaida (OC)	1,952,189,901.00	1,362,328,823.00	70
3.	Miradi ya Maendeleo	15,886,256,770.00	14,142,801,559.00	89
4.	Mapato ya ndani	9,545,811,000.00	8,559,970,557.00	90
Jumla kuu		**62,802,273,008.00**	**58,342,566,438.00**	**93**

2.1.2 Matumizi

Katika kipindi cha mwaka 2020/2021 Halmashauri ilipanga kutumia jumla ya **Tshs. 62,802,273,008.00** kwa kutekeleza shughuli mbalimbali za Maendeleo na Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya **Tshs 57,910,526,298.00** zilitumika kutoka vyanzo mbalimbali hii ni sawa na **92**% ya lengo kwa mchanganuo ufuatao**:-**

Machanganuo wa matumizi ya fedha za mwaka 2020/2021

Na	Chanzo	Makisio 2020/2021	Matumizi halisi 2020/2021	%
1.	Mishahara(PE)	35,418,015,337.00	34,277,465,500.00	97
2.	Matumizi ya Kawaida (OC)	1,952,189,901.00	1,342,389,462.00	69
3.	Miradi ya maendeleo (DEV)	15,886,256,770.00	14,130,172,663.00	89
4.	Mapato ya ndani	9,545,811,000.00	8,160,498,673.00	85
Jumla kuu		**62,802,273,008.00**	**57,910,526,298.00**	**92**

2.1.3 Mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka wa fedha 2020/2021

a) Kuendelea na ujenzi wa miradi ya Kimkakati ya Ujenzi wa Stendi ya Mabasi na Maegesho ya Malori katika eneo la Nyamhongolo ambapo kwa sasa kazi ya ujenzi imefikia 90%.
b) Kupitia fedha za EP4R Halmashauri imeweza kujenga na kukamilisha Ujenzi wa vyumba 15 vya madarasa katika shule za Msingi za Kayenze (3) Nyamadoke (2) Igogwe (3) Masemele (3) Nyamhongolo (3) na Kisundi (2). Pia

ujenzi wa matundu 36 ya vyoo na utengenezaji madawati 375 umefanyika katika shule za Msingi. Aidha kwa upande wa sekondari umefanyika ujenzi wa bweni 1, matundu 15 ya vyoo katika shule za Sangabuye (8) na Buswelu (7). Vilevile umefanyika ujenzi wa vyumba 5 vya madarasa katika shule za sekondari za Angelina Mabula (3) na Kayenze (2).

c) Halmashauri inaendelea na ujenzi wa vyumba vya madarasa 128 katika shule 24 za Sekondari ambapo Halmashauri imeweza kutumia jumla ya Tshs. 380,690,000/= kutoka mapato yake ya ndani kwa awamu ya kwanza.
d) Katika mwaka wa fedha 2020/2021 Halmashauri imepata ufaulu kwa 97.28% na kushika nafasi ya 2 Kimkoa na 6 Kitaifa katika mtihani wa darasa la saba sambamba na hilo pia ufaulu kwa upande wa elimu sekondari umeongezeka na kupunguza sifuri kwa asilimia 20% kutoka 60.39% hadi 39.60%. Aidha kumekuwa na ongezeko la daraja la kwanza kutoka 38.25% hadi 61.77% sawa na ongezeko la 23.54% na kumekuwa na ongezo la uandikishaji wa kidato cha kwanza.
e) Halmashauri imetumia fedha zake za ndani kununua madawa katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya, vilevile umefanyika upanuzi wa chumba cha kutolea huduma za mionzi katika kituo cha Afya Karume, upanuzi wa chumba cha maabara katika zahanati ya Kiloleli na ukamilishaji wa ujenzi wa Hospitali na uzio wake.

f) Halmashauri imeweza kununua generator ili kuendelea kuboresha utoaji wa huduma za upasuaji katika kituo cha Afya Buzuruga. Pia, kupitia wadau wa maendeleo chini ya mradi wa IMPACT Aghakhani wamekabidhi majengo 2 ya kujifungulia akinamama wajawazito yaliyopo katika zahanati ya Igogwe na Luhanga pamoja na jengo la upasuaji likiwa na vifaa vyake katika kituo cha Buzuruga.

2.1.4 Changamoto katika utekelezaji wa Mpango na Bajeti 2020/2021

Katika kutekeleza Mpango na Bajeti kwa mwaka 2020/2021, Halmashauri ya Manispaa ilikabiliwa na changamoto zifuatazo:-

a) Kutolewa fedha kidogo za Ruzuku ya Matumizi mengineyo na miradi ya maendeleo kutoka Serikali Kuu ikilinganishwa na Mpango kazi na Bajeti ya Halmashauri iliyoidhinishwa;
b) Mabadiliko ya tabia ya Nchi yaliyosababisha upungufu wa Samaki kwenye ziwa Victoria na hivyo kuathiri mapato ya ndani ya Halmashauri;
c) Mwitikio mdogo wa wananchi kuchangia shughuli za maendeleo; na

d) Uhaba wa watumishi hususani katika sekta za Afya, Utawala (Watendaji wa mitaa) na Elimu sekondari hususani kwa walimu wa masomo ya Sayansi.

3.1 MAPATO NA MATUMIZI KWA KIPINDI CHA MAPITIO YA BAJETI YA MWAKA 2021/2022 (JULAI – DESEMBA 2021/2022) KUISHIA DESEMBA, 2021.

3.1.1. **Mapato**

Katika kipindi cha Mwaka wa fedha 2021/2022 Halmashauri ilipanga kukusanya na kupokea jumla ya Tshs **74,910,906,197.00** kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbalimbali za Maendeleo na Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia tarehe 31 Desemba, 2021 jumla ya **Tshs 36,610,351,277.00** zilikusanywa/kupokelewa kutoka vyanzo mbalimbali hii ni sawa na **49% ya** lengo kwa mchanganuo ufuatao;**-**

Jedwali Na 1: Mapato ya Ndani Julai -Desemba Mwaka Fedha 2021/2022

Na	Chanzo	Makisio 2021/2022	Mapato Tshs (Julai - Desemba 2021/2022)	%
1.	Miradi ya Maendeleo (Ruzuku)	20,513,842,689.00	10,423,312,849.00	51
2.	Mishahara (PE)	42,496,789,508.00	19,565,282,332.00	46
3.	Matumizi ya Kawaida (OC)	1,727,568,000.00	1,580,733,860.00	92
4.	Mapato ya ndani	10,172,706,000.00	5,041,022,236.00	50
	Jumla	**74,910,906,197.00**	**36,610,351,277.00**	**49**

3.1.2 Matumizi

Katika kipindi Cha Mwaka wa Fedha 2021/2022 Halmashauri ilipanga kutumia jumla ya **Tshs. 74,910,906,197.00** kwa kutekeleza shughuli mbalimbali za Maendeleo na Matumizi ya kawaida. Hadi kufikia tarehe 31 Desemba jumla ya **Tshs. 33,733,378,286.00** zilitumika kutoka vyanzo mbalimbali hii ni sawa na **45%** ya lengo kwa mchanganuo ufuatao**:-**

Jedwali Na2: Matumizi ya fedha Julai -Desemba mwaka 2021/2022

Na	Chanzo	Makisio	Matumizi Tshs (Julai - Desemba 2021/2022)	%
1.	Miradi ya Maendeleo (Ruzuku)	20,513,842,689.00	7,672,511,090.00	37
2.	Mishahara PE	42,496,789,508.00	19,552,491,332.00	46
3.	Matumizi ya Kawaida (OC)	1,727,568,000.00	1,546,781,104.00	90
4.	Mapatoya ndani	10,172,706,000.00	4,961,594,760.00	49
JUMLA		**74,910,906,197.00**	**33,733,378,286.00**	**45**

3.1.3 MAFANIKIO

Mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka 2021/2022 ***(Julai – Desemba, 2021)***

i. Kuongezeka kwa vyumba vya madarasa 97, viti na meza 4,850 na ofisi 28 katika shule 26 za sekondari zilizojengwa kwa fedha za Mpango Wa Maendeleo Kwa Ustawi Na Mapambano Dhidi Ya UVIKO 19.

ii. Ujenzi wa vyumba 6 vya maabara katika shule ya sekondari Kirumba, Angelina Mabula, Mwinuko, Kabuhoro, Kayenze na Ibungilo.

iii. Ujenzi wa matundu ya vyoo 48 katika shule ya sekondari ya Kitangiri, Lumala, Nyamanoro na Kirumba kwa mapato ya ndani.

iv. Ujenzi wa mfumo wa kunawia mikono katika shule ya Sekondari Nyamanoro

v. Ujenzi wa vyumba 6 vya madarasa na viti 240 katika shule ya sekondari Kangaye, Nyamanoro na Kangaye kwa fedha za Lipa kutokana na matokeo (BRN).

vi. Halmashauri imefanikiwa kusimamia na kuendesha Mtihani wa Kuhitimu Elimu ya Msingi (PSLE) 2021, katika mtihani huo Halmashauri ilishika nafasi ya 2 Kimkoa na nafasi ya 7 Kitaifa kwa ufaulu wa asilimia 96.9.

vii. Uchaguzi wa wanafunzi wanaojiunga na kidato cha kwanza 2022 (selection) jumla ya wanafunzi 10393 wamechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza sawa na 100% ya ufaulu.

viii. Halmashuri imesimamia kwa kikamilifu ujenzi na ukamilishaji wa miundombinu na utengenezaji wa madawati kwa shule za msingi yenye thamani ya Tsh. 372,031,259.70. Jumla ya vyumba vya madarasa 32, matundu 6 ya vyoo na madawati 400 yametengenezwa kwa kipindi cha kuanzia Julai hadi Desemba 2021.

ix. Halmashauri ya Manispaa Ilemela imekua ikishiriki kikamilifu katika shughuli za Michezo kwa kuhamasisha, kuibua na kuendeleza vipaji vya watoto, kupitia vituo vya michezo (Sports Accademy), kuanzishwa kwa Jogging Clab ya Ilemela, kutokana na mahusiano mazuri na wafadhili tumefanikiwa kugawa mipira ya michezo mbalimbali kwa shule za Msingi na Sekondari zote za Manispaa Ilemela.

x. Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela inatoa elimu maalum kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu kupitia shule zenye vitengo na shule jumuishi (Inclusive). Katika kipindi cha kuanzia Julai 2021 hadi Desemba 2021 zimeongezeka shule 3 zenye vitengo vya Elimu maalum ambavyo ni Nyamhongolo, Buzuruga na Nyasaka na kufikia shule 10 zenye vitengo vya Elimu Maalum.

xi. Halmashauri pia imefanikiwa kuboresha huduma za afya kwa kujenga zahanati Lumala Masele na Nyandoke na ujenzi wa wodi 3 za wanaume, wanawake na watoto katika hospitali ya wilaya.

xii. Halmashauri inaendelea kuhamasisha wananchi juu ya kujikinga na ugonjwa wa UVIKO -19 ambapo wananchi wametambua njia mbalimbali ya kujilinda na ugonjwa huo.

xiii. Utambuzi wa mipaka ya migogoro ya Ardhi umefanyika kati ya eneo la Jeshi, Kikosi cha Anga na Uwanja wa ndege.

xiv. Halmashauri imeweza kulipa fidia kiasi cha Tshs. 61,813,912.00 katika eneo la barabara ya Buswelu center, eneo la shule ya Sekondari Lumala na eneo la Mradi wa Nyafula

xv. Halmashauri imeweza kuandaa hati miliki 1,482 na kutolewa kwa waombaji, pia "Deed Plan" 1152 zimeandaliwa kwa ajili ya uandaaji wa Hati Miliki katika viwanja mbalimbali.

xvi. Halmashauri imeweza kukusanya madhuhuri ya Serikali zinazotokana na kodi ya Ardhi ambapo kiasi cha Tshs. 1,496,705,791.16 kimekusanywa.

xvii. Halmashauri imeendelea kutekeleza eneo la mradi wa ujenzi wa stendi ya Mabasi na Maegesho ya malori Nyamhongolo ambapo ujenzi umefikia asilimia 97% sambamba na jengo la utawala ambapo ujenzi umefikia asilia 60%.

3.1.3.2. CHANGAMOTO NA MIKAKATI

3.1.3.3. Changamoto

Pamoja na mafanikio katika baadhi ya maeneo, Halmashauri yetu bado inakabiliwa na changamoto nyingi zikiwemo:-

NA	CHANGAMOTO	MKAKATI
1.	Kukosekana kwa vitendea kazi hasa magari yatakayotumika kwa ajili ya kufanya shughuli mbalimbali za maendeleo.	Hadi sasa katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 Halmashauri imefanya manunuzi ya magari 4 ili kupunguza upungufu huo. Pia katika Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2022/2023, Halmashauri imeendelea kutenga jumla ya Tshs 450,000,000.00 kwa ajili ya ununuzi wa magari 3 yatakayotumika kutekeleza shughuli mbalimbali za maendeleo.

NA	CHANGAMOTO	MKAKATI
2.	Uhaba wa watumishi hususani katika sekta za Afya, Utawala (Watendaji wa mitaa) Wahandisi na walimu hususani kwa walimu wa masomo ya Sayansi kwa upande wa Elimu sekondari.	Halmashauri inaendelea kutenga watumishi katika ikama kulingana na mahitaji ya sekta husika. Hata hivyo Halmashauri inaendelea kuomba Serikali Kuu kuleta watumishi kulingana na Ikama iliyoidhinishwa katika Mpango na Bajeti kwani mpaka sasa kuna watumishi 54 watendaji wa mitaa wameajiriwa kati yao watendaji wa mitaa 51 wameajiriwa kwa muda na 3 wameajiriwa katika ajira ya kudumu ili kurahisisha utendaji.
3.	Mwamko mdogo wa jamii kuchangia utekelezaji wa miradi ya maendeleo;	Halmashauri inaendelea na kutoa elimu kwa wananchi katika zoezi la O& OD, vikao na mikutano juu ya umuhimu kuchangia katika miradi ya maendeleo.
4.	Uhaba wa miundombinu shule za Msingi na Sekondari	Halmashauri inaendelea na ujenzi wa miundombinu ya shule ikiwa ni pamoja na ujenzi wa vyumba vya madarasa, matundu ya vyoo, vyumba vya maabara, ofisi, mabweni na utengenezaji wa viti meza na madawati. Aidha, Katika Mwaka Fedha 2022/2023 Halmashauri imeendelea kutenga fedha kwenye Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2022/2023 ambapo jumla ya Tsh 1,171,581,500.00 zimetengwa kwa ajili ya kazi hiyo.
5.	Kukosekana kwa fedha za fidia kwa ajili ya maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na Tasisi za umma, maeneo ya miradi na jamii kwa ujumla.	Halmashauri kuendelea kutenga fedha kwa ajili kulipa fidia ambapo jumla ya Tsh.1,000,000,000/= zimetengwa kutoka mapato ya ndani kwa ajili ya fidia. Aidha, halmashauri imepokea kiasi cha Tshs 3,000,000,000.00 kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya kulipa fidia katika eneo la Mradi Nyafula.

4.0. Muhtasari wa Vipaumbele vya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2022/2023

MUHTASARI WA VIPAUMBELE VYA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA 2022/2023				
NA	**SEKTA**	**SHUGHULI ZITAKAZOTEKELEZWA**	**CHANZO CHA FEDHA KILICHOTENGWA**	
			MAPATO YA NDANI	**FEDHA KUTOKA SERIKALI KUU**
1.	**UJENZI**	Ujenzi wa barabara km.1.5 kwa kiwango cha lami, matengenezo ya kawaida katika maeneo korofi km. 200 katika kata 19, matengenezo ya taa za barabarani, na kufanya upembuzi yakinifu kwa miradi iliyotekelezwa kupitia TACTIC na kufanya ukamilishaji wa mradi wa mabasi Nyamhongolo.	1,338,572,600.00	6,000,000,000.00
2.	ELIMU SEKONDARI	Ukamilishaji wa vyumba 60 vya madarasa, Maabara na Bweni katika shule ya sekondari 27 katika Manispaa ya Ilemela.	350,000,000.00	4,836,114296.00
3.	MAENDELEO YA JAMII	Kuwezesha vikundi 226 kiuchumi kwa kutoa mikopo isiyokuwa na riba kwa vikundi 93 vya wanawake wajasiriamali, Vijana 93 na vikundi vya watu wenye ulemavu 40 kwa ajili ya kuongeza tija katika shughuli zao. Kuimairisha kamati 10 za kudhibiti UKIMWI ngazi ya Kata na kuwezesha makundi yasiyojiweza kiuchumi kupitia TASAF.	1,323,061,240.00	2,930,097,000.00
4.	AFYA	Kuboresha huduma za Afya kwa kukamilisha ujenzi wa Hospitali ya wilaya, umaliziaji wa Zahanati 2 za Nyamadoke na Lumala Kituo cha Afya Nyamhongolo/Buswelu Vifaa tiba na dawa Samani na mitaa ya Ibungilo, Kanganja na Bezi na kusimamia shughuli za lishe. Ununuzi wa madawa, vifaa tiba na mapambano dhidi ya UKIMWI na Malaria.	802,702,316.00	3,192,214,498.17

MUHTASARI WA VIPAUMBELE VYA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA 2022/2023				
NA	**SEKTA**	**SHUGHULI ZITAKAZOTEKELEZWA**	**CHANZO CHA FEDHA KILICHOTENGWA**	
			MAPATO YA NDANI	**FEDHA KUTOKA SERIKALI KUU**
5.	ELIMU MSINGI	Ukamilishaji wa ujenzi wa vyumba 30 vya madarasa na utengenezaji wa madawati 1,000 katika shule za msingi.	475,000,000.00	1,105,109,500.00
6.	ARDHI NA MIPANGO MIJI	Kufanya uthamini na kulipa fidia maeneo mbalimbali ya Halmashauri ikiwa ni pamoja na barabara za Nyamhongolo standi - Nyamadoke - Buswelu na Coca cola - Busenga - Buswelu na fidia za Taasisi za Serikali na kuweka anwani za makazi kwenye nyumba 50,000 katika kata 19	1,000,000,000.00	-
7.	UTAWALA	Kuwezesha ujenzi wa ofisi mpya 2 za Watendaji Kata katika kata za Nyasaka na Buzuruga, ujenzi wa ofisi mpya 8 za Watendaji wa Mitaa katika mitaa ya Bezi, Bwiru Bima, NHC Magharibi, Kilimahewa A, Mlimani B, Kawekamo B, Kileleni na Nyamanoro B. Ununuzi wa magari 3 na pikipiki 12 kwa Watendaji Kata wa Nyakato, Mecco, Buzuruga, Ibungilo, Nyamanoro, Kirumba, Kitangiri, Pasiansi, Kawekamo, Ilemela, Kiseke na Buswelu.	670,000,000.00	1,000,000,000.00
8	MIPANGO TAKWIMU NA UFUATILIAJI	Kuendelea kutekeleza shughuli za uibuaji wa Fursa na Vikwazo katika Maendeleo (O & OD), kulipa madeni, kufanya maandiko mbalimbali ya miradi, kununua regista za makazi na kuboresha Makala ya Kiuchumi na Kijamii ya Wilaya	500,000,000.00	60,396,000.00
9.	MIFUGO NA UVUVI	Ununuzi wa Fiber boat, Ujenzi wa machinjio ya nguruwe, Ufugaji wa samaki, na Uboreshaji wa mialo	400,000,000.00	-
10.	USAFISHAJI NA	Kuwezesha ununuzi wa gari 1 la kusafirisha taka ngumu na mabirika	282,514,284.00	-

MUHTASARI WA VIPAUMBELE VYA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA 2022/2023				
NA	**SEKTA**	**SHUGHULI ZITAKAZOTEKELEZWA**	**CHANZO CHA FEDHA KILICHOTENGWA**	
			MAPATO YA NDANI	**FEDHA KUTOKA SERIKALI KUU**
	MAZINGIRA	(skip buckets 4)		
11.	FEDHA NA BIASHARA	Ukarabati wa vyoo 10 vya Buzuruga, Sabasaba, Nyakato, Pasiansi, Buswelu, Kirumba, Msuka na Kiloleli na kuboresha miundombinu ya masoko 10 ya Buzuruga, Nyakato Mbao, Msuka, Pasiansi, Nyamanoro, Sabasaba, Kiloleli, Buswelu, Nyasaka A na B	150,000,000.00	-
12.	KILIMO UMWAGILI AJI NA USHIRIKA	Kuviwezesha vikundi 7 vya wakulima wa mazao ya bustani mfumo rafiki wa umwagiliaj Kukipatia kituo cha mafunzo cha Sangabuye vifaa na zana kwa ajili ya Ward Resource Centre (WRC na ujenzi wa jengo la kusindikia unga wa mhogo kikundi cha KKN-kata ya Kayenze	90,000,000.00	-
13.	TEHAMA	Kuboresha miundo mbinu ya TEHAMA katika maeneo malimbali ya Halmashauri	80,000,000.00	-
14.	NYUKI	Kuwezesha vikundi 4 vya ufugaji nyuki juu ya upatikaji wa masoko ya mazao ya nyuki Kutengeneza mizinga 200 na kuigawa kwa vikundi 4 vya ufugaji	44,517,000.00	-
JUMLA			**7,506,367,440.00**	**19,123,931,294.17**

4.1. MIKAKATI YA KUONGEZA MAPATO

Katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Manispaa imeongeza jitihada katika vyanzo vya mapato kwa kufanya yafuatayo:-

a) Kubuni vyanzo vipya vya kuongeza mapato ikiwa ni pamoja na, ujenzi wa machinjio ya nguruwe, Mradi wa ufugaji samaki, ujenzi wa Kituo cha Biashara (Buzuruga Commercial Centre) katika eneo la standi ya Buzuruga

na kuimarisha miundombinu ya barabara eneo la mradi wa viwanda Nyamhongolo (Nyamhongolo Industrial Park)

b) Kuongeza nguvu katika ufuatiliaji wa mapato na kufanya ukaguzi wa mara kwa mara na wa kushitukiza ili kubaini mianya inayovujisha mapato.
c) Kuimarisha Mradi wa Mashine ya Ufyatuaji Tofali ili uweze kuzalisha tofali kwa tija,
d) Kuanza kutumika kwa Sheria ndogo za Halmashauri za Mapato ya ndani ili kufanya marekebisho ya viwango vya ushuru na kodi ya taka ya 30% kutekelezwa kwa wakati;
e) Kuendelea kutoa elimu ya Walipa kodi ili wafahamu umuhimu wa kulipa kodi. Pia kufanya agenda ya mapato kuwa ni ya kudumu katika vikao vya ngazi zote katika Manispaa;
f) Kuendelea kuimarisha Mfumo wa ukusanyaji, utunzaji Takwimu na kumbukumbu za walipa kodi kwa kuwabaini walipa kodi wote wakubwa na wadogo kwa ajili ya Kodi ya Huduma;
g) Kuchukua hatua zaidi za Kisheria kwa wanaoshindwa kulipa ada na tozo mbalimbali za Halmashauri;
h) Kuongeza idadi ya mashine za kielektroniki za kukusanyia mapato katika vyanzo vyote. Aidha, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 mashine za POS 90 zimenunuliwa.

4.2. MAOMBI MAALUM

Sambamba na uwasilishaji wa mapendekezo ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Halmashauri inawasilisha maombi maalumu yenye jumla ya **Tsh. 30,100,000,000/=** kama ifuatavyo;

i) Kuomba fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya katika Eneo la Kabusungu Tsh.16,000,000,000/=
j) Kuomba fedha Tshs 14,100,000,000.00 kwa ajili ya Kituo cha Kibiashara (Buzuruga Commercial Centre) katika eneo la standi ya Buzuruga.
k) Kuomba fedha Tsh.10,000,000,000/= kwa ajili ya kuimarisha miundombinu ya barabara eneo la mradi wa viwanda Nyamhongolo(Nyamhongolo Industrial Park)

5.0 HITIMISHO

Mhe. Mwenyekiti, Mpango na Bajeti hii imejadiliwa katika vikao vyote vya kisheria vya Halmashauri kwa mtiririko ufuatao:-

1. Kikao cha Timu ya Menejimenti kilichofanyika tarehe 18/01/2022
2. Kikao cha Kamati ya Ukimwi kilichofanyika tarehe 19/01/2022
3. Kikao cha Kamati ya Mipangomiji, Ujenzi na Mazingira kilichofanyika tarehe 20/01/2022
4. Kikao cha Kamati ya Huduma za Uchumi, Afya na Elimu kilichofanyika tarehe 21/01/2022

5. Kikao cha Kamati ya Fedha na Uongozi kilichofanyika tarehe 22/01/2022
6. Kikao cha Baraza la Wafanyakazi kilichofanyika tarehe 24/01/2021.

Mhe. Mwenyekiti, Kupitia vikao hivyo Halmashauri iliweza kupata maoni ya wajumbe ambayo yalizingatiwa katika kuboresha bajeti na kuweza kupata Mpango na Bajeti iliyoshirikishi zaidi. Maoni ya vikao hivyo yamejumuishwa katika Mpango na Bajeti hii.

Aidha, Baada ya kusema hayo, naomba sasa Baraza lako liweze kupokea na kupitisha Mpango na Bajeti ya Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2022/2023 yenye Jumla ya **Tshs 77,194,840,806.17** kati ya fedha hizo **Tshs** 19,123,931,294.17 ni kwa ajili ya Ruzuku ya Miradi ya Maendeleo, Tshs 42,819,341,512.00 ni Mishahara(PE), **Tshs** 1,727,568,000.00 Ruzuku ya Matumizi ya Kawaida kutoka Serikali Kuu(OC) na **Tshs** 13,524,000,000.00 ni mapato ya ndani(Own Source) ambapo **Tshs 7,506,367,440.00** kati ya fedha hizo ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo na Tshs **5,004,244,960.00** ni matumizi ya kawaida na Tshs 1,013,387,600.00 ni mapato Fungwa(Restricted Fund) yanayotokana na mapato ya ndani kama jedwali linavyoonesha hapa chini**:-**

Jedwali Na3: Makisio ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2022/2023

Na	Chanzo	Makisio Tshs 2022/2023	%
1	Miradi ya Maendeleo	19,123,931,294.17	25
2	Mishahara (PE)	42,819,341,512.00	55
3	Matumizi ya Kawaida (OC)	1,727,568,000.00	2
4	Mapato ya ndani	13,524,000,000.00	18
Jumla		**77,194,840,806.17**	**100**

Naomba kuwasilisha,

Eng: Modest J. Apolinary
MKURUGENZI WA MANISPAA
ILEMELA